



**RECORDINGS OF CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS OF MUMIAS CONSTITUENCY HELD AT ST.**

**BEDAS BUKAYA SECONDARY SCHOOL**

**ON 29<sup>TH</sup> JULY 2002**

**PRESENT**

**Com. Riunga Raiji** – in chair

**Com. Salome Muigai**

**Com. Dr. Mohammed Swazuri**

**SECRETARIAT IN ATTENDANCE**

John Watibini	Program Officer
Gladys Gichuki	Asst. Program Officer
Asha Bor	Verbatim Recorder
Anne Nambiro	District Coordinator

**The Meeting started at 10.00 a.m. with Com. Raiji in the chair.**

.....mmoja wenu atuongoze kwa maombi.

**Rosenail Obonyo:** Natuombe. Baba katika jina la Yesu, tunakuita sasa hivi Mungu wetu kwa sababu umetuwezesha kufika siku ya leo, siku ambayo tumeongoja sana. Baba tunasema asante, asante kwa kuleta wageni ambao wamekuja kuchukua maoni yetu baba. Tunakuomba ukae kati yetu wakati tunaanza, hata wale hawajafika Mungu wangu, tunaomba uwaletе kwa haraka ili tuendeleе pamoja. Asante kwa serikali yetu, asante kwa Rais wetu ambaye ametupatia nafasi hii tutoe maoni yetu ambayo itatusadia hata na watoto wetu na wajukuu wetu. Baba tunaomba uzidi kutuongoza kwa hiki kikao baba. Tukimaliza vizuri vile tutaanza vizuru, tutakushukuru Baba. Naomba katika jina la Yesu kiongozi wetu. Amen.

**Com. Raiji:** Asante sana mama. Kwa niaba ya tume ya kurekebisha katiba, ninafuraha kuwakaribisha nyinyi nyote katika kikao hiki rasmi cha tume. Kabla hatujaanza, ningetaka tujue tuko na Commissioners wagani ambao wametumwa hapa na tume na nitawauliza muwaambie majina yao nikianza upande huu wangu wa kulia.

**Com. Salome Muigai:** Hamjambo watu wa Mumias

**Audience:** Hatujambo

**Com. Salome Muigai:** Mimi naitwa Salome Wairimu Muigai na ni furaha kubwa kuwa nanyi leo.

**Com. Swazuri:** Habari ya asubuhi?

**Audience:** Mzuri

**Com. Swazuri:** Mimi naitwa Mohammed Swazuri.

**Com. Raiji:** Na mimi jina langu ni Riunga Raiji na mimi ndio nitakuwa Mwenye Kiti wa kikao cha siku ya leo. Pamoja na ma-Commissioners hawa wako mbele yenu hapa watatu. Tuko na maofisa wengine kutoka makao makuu ya Tume. Tuko na Bwana John Watibini ambaye ni Programme Officer.

**John Watibini:** Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo

**Com. Raiji:** Tuko na Bi. Asha Boru ambaye ni Verbatim Recorder

**Asha Boru:** Hamjambo?

**Com. Raiji:** Tuko na Gladys Gichuki ambaye ni Assistant Program Officer. Na pia tuko na District Coordinator na wana chama wa Constituency Committee na nitamuuliza District Coordinator aje hapa atujulishe tu kwa majina wale wanachama wa threeCs ambao wako hapa ambao wamekuwa wakitayarisha na kufanya kazi kubwa ili kutayarisha mambo ya siku ya leo.

**Anne Nambiro:** Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Anne Nambiro:** Tuko na wanakamati wa katiba ya (inaudible) hapa wanne na nitaanza na Mwenye Kiti, Acting Chairman. Jina lako tafadhali na jambo.

**Peter Sakwa:** Peter Sakwa. Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Anne Nambiro:** Mwenye anatumfuata ni secretary

**Rita Katamwa:** Rita Katamwa. Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Anne Nambiro:** Mwenye anatumfuata ni member

**Abdangwa Shikanga:** Abdangwa Shikanga. Hamjambo nyote?

**Audience:** Hatujambo.

**Anne Nambiro:** Next, member

**Janet Ayeta:** Janet Ayeta ni member. Habari zenu wote?

**Audience:** Njema

**Janet Ayeta:** Mwakaribishwa

**Audience:** Asante

**Anne Nambiro:** Na mimi ndiye District Coordinator, Ann Nambiro. Asante kwa kufika.

**Com. Raiji:** Asante sana Anne. Kwanza kabisa kabla hatujaanza tungetaka kuwajulisha utaratibu ambao utakuwa katika kutoa maoni. Kwanza kama mnavyojua, hiki ni kikao rasmi cha tume kwa hivyo wakati munatupatia mapendekezo yenu, mtakuwa mkipatia Tume na kila mtu yuko huru kupendekeza mambo yote anayofikiria itatusaidia katika kurekebisha katiba. La pili, tutatumia lugha zetu rasmi, Kiingereza na Kiswahili lakini kama hujui hizo lugha, uko huru kutumia lugha ya mama na nafikiri Ann atatumia mtu wa kututafsiria.

Kuna jinsi tatu za kutoa maoni. Kwanza kabisa unaweza kutupatia nakala au memorandum ambayo umeandika bila kusema neno lolote, utatumia kwa sababu hapa ndio ofisi yetu. Tutaandika, tutaipokea na tutaitumia wakati wa kuiandika ripoti ya

kurekebisha katiba. Unaweza kuwa na memorandum lakini ungetaka tu kuzungumza maneno machache. Utapatiwa dakika tano kutupatia tu summary au highlights kwa sababu ya masaa hatuwezi kukubalia mtu asome memorandum yote kwa sababu ingine ni ndefu sana kwa hivyo, utapatiwa dakika tano utupatie tu yale muhimu kwa sababu memorandum yenyewe tutaenda nayo na tutapitia wakati tunarekebisha katiba.

Jinsi ya tatu, unaweza kuwa huna maandishi yoyote lakini unataka kunena mapendekezo yako. Uko huru kufanya hivyo na pia utapatiwa dakika tano ili sasa ututolee mapendekezo. Ningemuomba wakati mnakuja hapa muwe mkitupa mapendekezo, recommendations or proposals kwa sababu hizo ndizo tunataka ili tuzitumie kurekebisha katiba. Kwa hivyo ma-story ndefu sana sana kwa hivyo, jaribu kuleta point yenyewe ili utumie saa yako vizuri. Pia, baada ya kutoa maoni yako, ma-Commissioners wako huru kukuliza upanulie jambo fulani ambalo labda hawajaelewa ama kupata sawa sawa. Kwa hivyo utangoja kidogo kama kuna maswali ama kitu cha kufafanua, utaulizwa lakini ningetaka kuwajulisha kwamba ma-Commissioners hawako hapa kujadiliana na nyinyi. Kazi yetu kama Commissioners ni kusikia na kupokea maoni yenu. Maoni yote mnatoa hapa tuna record, tuko na tape recorder kwa hivyo usiwe na hofu kwamba hayo mapendekezo yenu hapa labda hayatafika huko kwa Tume, yatafika.

Nafikiri hakuna mengi, tutaanza sasa na vile tunafanya ni kwamba tunaanza na mtu ambaye alijiandikisha mbele. Kwa hivyo tutafuata taratibu wa vile watu walifika lakini tukiona ni heri tunaweza kurukia ili tufikie labda watu kama wakina mama ama walemavu, wale ambao wako shuleni na kwa hivyo tutafuata orodha. Ukimaliza kutoa maoni yako au memorandum, tafadhali utaenda hapa ujiandikishe kwa sababu Tume inataka orodha rasmi ya wale waliotoa maoni ili wakitaka kuenda kuthibitisha, watakuwa huru kufanya hivyo. Asanteni.

Tutaanza na Celine Wesonga, Ukaya Student. Karibu. Wa pili tutampatia nafasi, Stephen Rabile Okuok. Stephen, Ukaya Teachers', yuko?

**Speaker:** (inaudible)

**Com. Raiji:** Yuko upande huo?

**Speaker:** Ndio.

**Com. Raiji:** Okay. Rowland Ombuge? Rowland eh?

**Speaker:** (inaudible)

**Com. Raiji:** Okay. Uko tayari kutoa yako?

**Speaker:** Niko nayo

**Com. Raiji:** We will give you five minutes to give us the highlights or summary. Please have a seat. Utaanza kwa kusema jina lako ili liingie kwa tape.

**Stephen Obok:** Hamjambo wote?

**Audience:** Hatujambo.

Kwa majina ni Stephen Obok. Nina maoni ya Waalimu wa St. Bedas Bukaya High School. Tumeandika kwa lugha ya Kimombo kwa hivyo nitasoma kwa lugha hiyo. Teachers from St. Bedas Bukaya Secondary School are proposing the following: -

- Nominated MPs should not be allowed to hold Ministerial post in the country.
- Even children be allowed to acquire or inherit their parents property especially land and other things.
- The President should not be the Chancellor of all public universities in Kenya instead they should appoint qualified personnel to that position.
- Basic education should be free and compulsory to all Kenyan children to eradicate illiteracy.
- They are also proposing the creation of post of a Prime Minister and reduce the powers of the President. They are saying that the Prime Minister should serve a maximum of two terms of five years each.
- Sentence for rapists should be made more harsh to reduce such incidences.
- Anybody who fails general elections should not be nominated as an MP. A person who attempts to vie for either MP or President twice unsuccessfully should not be allowed to vie any other time.
- MPs and Chiefs or leaders should be answerable to what development progress has been achieved during their time and why and how it has been achieved otherwise they will drop if they cannot explain.
- Agriculture being one of the most important sectors, it should be well addressed in the Constitution to enhance productivity. Actions, which may lead to poor production that is stealing from other people's funds or mismanagement of products, should be addressed.
- All parents should give proper care to their children according to their abilities.
- The scrapping of nomination of MPs and councillors.
- All MPs be involved in the proroguing and dissolution of Parliament. It should not be left to the preserve of the President.
- There is a suggestion that they should have two Chambers in the House, that is the House of Common for elected representatives and the Senate made up of retired senior citizens from various professions like law, medicine and

engineering just to name a few.

- They are also suggesting that we create a federal system of government with five governors in this manner; Western, Central, Rift Valley, Eastern and Coast.
- There is a suggestion that all nursery school teachers to be employed by TSC instead of community.
- The government to train and post guiding and counselling personnel to schools to counsel teachers and students.
- We naturalize the citizens born of Kenyan mothers and alien fathers.
- The delegate system of voting should be done away with. Ceremonial positions like Mayors be scrapped. Selection to middle level colleges should be done away with.
- All sub Chiefs and Chiefs should be of 'O' level education and above and have a certificate or diploma in Public Relations and they be paid well to avoid corruption.
- Teachers in a given situation should elect their heads whenever vacancy arises.
- Interdiction for teachers should be decided by all teachers before the Principal or BOG, that is to say a disciplinary council made up of teachers and they should be part of the policy makers. Ministries should not be headed by MPs but by specialists that is people with education that pertains to that Ministry.
- The Constitution should give room where the voters who are the employers of the MP to have a vote of no confidence to their MPs if they fail to work as expected.
- The President should not be an MP, he or she should be an independent Kenyan and not attached as a Member of Parliament in any constituency.
- Presidential elections to be carried out separately from MP elections and even civil elections. The President should not be a Commander-in-Chief of the Armed Forces and finally they are suggesting that we should abolish political inheritance. Thank you

**Com. Raiji:** Thank you very much Stephen. Register yourself. Celine Wesonga. That was the student. Welcome.

**Speaker:** You can have a sit there.

**Celine Wesonga:** Our teachers and our visitors, this morning...

**Com. Raiji:** (inaudible). Start with your name please so that we can record.

**Celine Wesonga:** I am Celine Wesonga. This morning I am going to talk about the roles of women in Kenya today and we tried to come up with the following report.

- Women should be allowed to inherit land. The government should announce that publicly so that all the people in Kenya are aware of that.
- Second, women should have that right to marry men. By this we mean, instead of the men taking the women to their

home, even the women should take the men to their homes.

- Another point is that the government should make an appointment to ensure that all women in Kenya wear long dresses. It must be compulsory.
- There should be equality in job opportunities for both men and women. If a man can be a pilot, why can't a woman become a pilot? If he can make to be a caretaker same to a woman then a makanga (tout).
- The government should announce publicly that every family must give birth to a maximum of six children, more than that may lead to jailing both the woman and the man and then a minimum of three children.
- All men rapists to be castrated or jailed for life and it should be announced publicly and on a serious note.
- All thieves should not be jailed to die there, instead they should be cut the limbs, they should be cut. You cut both the legs and the hands so that they will know that, I stole and that is why I do not have these limbs. Thank you.

**Com. Salome Muigai:** We need to get some clarification. Thank you very much Celine, those were very important prepositions. I just have a few questions for you. You are talking about equality of men and women and at the same time, you are saying women should wear only long clothes. Could you explain to us what you mean by women wearing long dresses? My other question is on the limbs. There are people born without limbs so when you say that all thieves will be known that they stole and that is why they have no limbs. What happens to those who are born without limbs, those whose limbs are cut because of some diseases? Will they have to share thought because they stole or how will you tell the difference?

**Celine Wesonga:** Thank you. First, I will tackle the question about putting on of long dresses. If the government makes it to be known that all women should put on long dresses, we are not going to get cases of maybe girls being raped because of the short skirts they are putting on or mini skirts or the tights they normally put on. So, Kenyans must be identified to be putting on long dresses. If you go to Nigeria, you will get that putting on 'vitenges' identifies these women they are long and smart. If you see a Nigerian woman and you are educated, you will not fail to know that woman so the women should just put on long dresses.

For the thieves, if someone was born without limbs, that one is automatically known and if someone is a thief and you cut him or her, the family. You know most of the people do inherit the theft from the family so in this case you will get that the same family has almost three thieves and if a brother is cut, the two are going to change.

**Com. Raiji:** Thank you very much (inaudible). Tell us your names.

**Mohammed Odongo:** My names are Mohammed Odongo.

**Com. Raiji:** You have to say your school for the record.



**Mohammed Odongo:** From St. Bedas Bukaya Secondary School.

**Com. Raiji:** Endelea mbele.

**Mohammed Odongo:** The students have come up with some views. The first one was that people should elect the Mayors and the councilors because they are the ones who can specify who or which person fits a particular post. Secondly, we feel that the council officials, the Mayors and councillors should not serve for only two years; they should serve for the normal five years so that as Parliament is dissolved, all of them are retrenched to get new ones in the new government. Another thing is that the maximum serving time should be five years after which the retrenched officer should not again be allowed to be voted for so as to have equal (inaudible) of the nation of Kenya. The election dates for each five-year plan should be specified in the Constitution so that campaigning becomes fair and the citizens be well prepared on who to cast their votes for. Apart from winning the votes, the President and other elected civil servants should fulfill the following qualifications. He should be morally upright, at least a form four graduate and a Kenyan citizen.

The multi-functions of President should not exist in the new Constitution; he should only be a President and an MP. Others such as Commander-in-Chief and chancellor of universities should not be allocated to such persons so that others can get the job and avail the opportunities to many Kenyans. There should not exist nominated or very special Ministers but all of them should be elected by the citizens, not just to push them there and ask the citizens they have been taken.

All the civil servants should only concentrate on one job so as to avail other similar chances to the organs of the country. During the voting, the second person after the President should become the Vice President and in case she or he suits the required qualifications but if not, then anyone who has gone for post but failed should be made the Vice President.

A Kenyan citizen caught for breaking the law should just be arrested but should not be whipped or subjected to any form of disciplinary action. He should just be guided and counselled and if possible, be given strategic post in the process of nation development. For example, he can be taken to polytechnics or any other training institutions nearby.

Death penalty should be abolished completely. The current Constitution does not protect full employment for the citizen properly. For example, in Western Kenya, sugarcane as the only cash crop does not presently encourage farmers to plant it. When inputs should be brought to the farm and that process done there. The expense of some get lost on the way to the factory should be the responsibility of the company and the one to suffer but not the farmers.

On education, there is unfair distribution of education resources. Schools which are known for performing well and which are able are being made more able living the cheap ones like our school Bukaya behind. How can you prove education you say that by then yet there is unfair distribution. Also, unable students have just been left to drop out of school due to school fees.

Students also lose their hope because compared to the old systems in schools with the present ones you see there is a great difference. In old schools, milk was being brought to the schools. Pens and books were donated to the school by the government but are they there today? Are we really going ahead or we are backsliding?

**Com. Raiji:** You have a long memorandum, we will collect it. Just summarize the rest and you have one and a half minutes.

**Mohammed Odongo:** Another thing is that education should be made compulsory for any person below 18 years of age and any person found roaming on the streets yet is supposed to be in school should just be repatriated to the village. The teachers should be fitted with uniforms so as to identify them quite easily and anybody or any public servant found on duty with no proper uniform should be given a compulsory leave or suspended for a month. Students should not be given any form of punishment while in school. Proper guiding and counseling should be given to them and the any teacher found violent with students should be suspended for a month. Kenyans should be made aware of anything going out of the country. They should be accessed this information to the possession of the state or any other agency, organ of the State.

Finally, for day schools it should be very clear that any student who is able or willing to stay in the school should be given the chance so that he can gain like the other national schools does.

**Com. Raiji:** Asante sana. Can you get yourself registered. Mr. Rowland Ombuge I think that is the Principal. Karibu sana.

**Speaker:** Excuse me Sir, do you want to hand over your document?

**Com. Raiji:** Yes, you are free. If you have a written memorandum, you are free to get it registered and then you are released. You do not have to read it all. Thank you. Mwalimu if you could start with your name first.

**Rowland Ombuge:** Majina yangu kamili ni Mwalimu Mkuu wa St. Bendas Bukaya, Mukumu (inaudible). Nafikiri niliulizwa swali ya kata ndogo ya Bukaya. Wazee walikutana hapa na wakapendekeza maoni fulani ambayo waliniuliza nisome kwa niaba yao. Tulipitia pengine yote ambayo ilikuwa ya mijadala ya uma na tukapendekeza mambo machache, kwa hivyo ningependa kuanza kwa kusema kwamba, katika utangulizi wa katiba yetu, wakaazi wa Bukaya walipendekeza kwamba katiba yetu mpya iwe na utangulizi huku ukieleza umuhimu wa taifa, umoja, heshima ya katiba, kuheshimu kazi na tamaduni za makabila yote ya Kenya, haki ya kumiliki mali, uzozaji wa raslimali, haki za watoto, wamama, wazee na walemavu, haki za kuabudu na utaratibu wa kusajili madhehebu, idadi ya vyama vya kisiasa, haki za vyama vya ushirika na wafanyi biashara rejareja, haki ya elimu, maji masafi, uhifadhi wa misitu na mazingira. Kwa hivyo walitarajia mambo ya katiba yetu ikiwa na utangulizi wa aina hiyo itakuwa na mwelekeo.

Kuhusu kanuni za kuongoza sera za serikali, mambo muhimu ambayo waliwahi kuguzia ni kuhusu wazee. Maoni ya wazee hasa

kuhusu maisha yaweze kutiliwa maanani sana katika katiba yetu kwa sababu siku hizi wanaonelea kwamba wanaanza kupuuza. Swala la mama kambo na baba kamba walisema pia haliko kwa desturi za mwafrika kwa sababu huharibu, inaondoa umoja wa jamii na pia huharibu taifa kwa hivyo walisema mambo kama haya yakiondolewa (inaudible).

Walisema kwamba Rais ambaye anakuja, kanuni zake za siku dumu ashtakiwe apate kustaafu na mawaziri wateuliwe kulingana na ujuzi wao katika idara hizi. Iwapo ni wajumber, wawe wana degree. Baada ya uchaguzi iwapo tutategemea serikali ya mseto, wamependekeza kwamba pawe na viama vinne pekee vya kisiasa na pia viama hivyo iwapo vitaunda serikali ya mseto, kile kinachoshinda na hakina waMbunge wa kutosha kimtoe Rais na kile cha pili kimtoe Waziri Mkuu, cha tatu makamu wa Rais na cha nne Waziri Mkuu mdogo. Hivyo ndivyo kuunda serikali ya mseto ambayo itakuwa na utafa maalum. Pia walizungumzia ambayo tayari waalimu wamezungumzia kwamba Wabunge maalum wasiteuliwe kuwa mawaziri na wawachiwe kutetea wajibu walioteuliwa kwa mfano walipendekeza kwamba Wabunge maalum wateuliwe kutegemea makundi maalum kama vile walemavu, wale wenye ujuzi katika nyanja mbalimbali ili waweze kuwakilisha makundi hayo kuliko kuwateuwa watu ambao tayari wamewakilishwa kwingine.

Walisema kwamba wapewe muda wa kuongoza kwa vipindi vitatu vya miaka mitano. Wale ambao wanastaafu kutoka ambao umefanya kwa muda wa vipindi viwili walipwe marupurupu ya kustaafu. Wahuduma wengine wa serikali wanaostaafu walipwe marupurupu yao haraka na waongezwe kutoka miaka kumi na tano hadi ishirini na tano, wale wafanyikazi wa serikali. Marekebisho pia yafanyiwe malipo ya uzeeni ili yalingane na hali ya kiuchumi kwa sababu wengine bado wanalipwa ujira mdogo.

Kuhusu uwezo wa katiba, walipendekeza kwamba katiba isiruhusu Wabunge kubadilisha (inaudible) fulani fulani vya sheria bila kuwashauri wananchi walioshiriki katika kuunda katiba. pia walipendeza katiba imruhusu Rais kuteuwa kamati inayoidhinisho la Bunge ili kuongoza mkutano wa kubadili katiba iwapo kuna haja ya kufanya hivyo.

Kuhusu uraia jambo ambalo lilitokea sana ni kuhusu yale mengine wamezungumzia lakini walisema kwamba iwapo mama ameoleka kwingineko na arejee hapa Kenya na ni Mkenya, akija na wanawe, watoto hao wapewe uraia wa Kenya kwa muda wa miaka mitano huku wakiangalia iwapo patakuwa na kurudiana au mda huo unaweza kuongezwa kutegemea vile hali ilivyo ki-ndoa na iwapo mke anaolewa akiwa mja mzito, basi baba achukue jukumu la yule mtoto aliyezaliwa au mtoto anayeandamana na mtoto huyo na apewe haki yake ya kuridhi. Walisema kwamba vyeti vya kuzaliwa vitiliwe maanani kumtambua raia wa Kenya na jukumu ya raia yategemee namna uraia ulivyopatikana na katiba isiruhusu raia wa nchi mbili kwa sababu inaweza kuzusha vitendo vya ugaidi au kupeleleza kwa niaba ya nchi zingine.

Ulinzi na usalama; walipendekeza vikosi vyote vya silaha viguzwe na katiba. amri jeshi abakie Rais lakini kutangaza vita, pawe na kamati ya ulinzi na usalama ya kumshauri Rais. Polisi wanapofanya msako wa vijijini kutafuta pombe haramu au madawa wa kulevya waandamane na wazee wa mtaa. Wazee wa vijiji waajiriwe na serikali ili kutekeleza kazi yao vyema na walipwe ujira.

Katiba iruhusu uwezo wa kipekee katika hali ya hatari kama vile vita, majanga ya kitaifa, maasi na kukosekana kabisa kwa usalama na mamlaka haya watumiwe na kamati ya usalama ikiongozwa na Rais.

Ningependa kumalizia kwa sababu nimesema kwamba mambo haya yameandikwa na ndio maana huoni watu wengi hapa. Wengi walikuwa wamezungumzia na tukayaweka pamoja kwa hivyo mengi mtayapitia lakini muundo wa (inaudible) ya serikali wamependekeza tutazidi kuwa na vyama vingi. Kuhusu Bunge wamependekeza kwamba Wabunge wasihamehame kutoka chama kimoja hadi kingine wakati wanahudumu kwa miaka mitano na kuhusu mamlaka ya nchi, lazima katiba iweke takiriba ya Rais atakayeteuliwa.

Mahakama, jambo ambalo lilijitokeza muhimu sana ni kwamba pawe na mahakama ya katiba na pia mahakama ya juu halafu mahakimu wastaafu baada ya miaka sitini sio sabini na mbili. Katiba ichunguze wale mawakili ambao huwafuja raia na wale wanawakilisha jamaa zao kwenye mahakama ambao wanaipotosha mahakama. Kwa hivyo katiba itoe mamlaka kuwaachisha au kuwanyang'anya. Walisisitiza serikali za wilaya zipewe haki ya kusimamia raslimali katika sehemu zao ili waweze kuorodhesha matumizi hayo. Kuhusu mfumo wa utaratibu wa uchaguzi, walisema kwamba ma-Commissioner wawe twofive na wawe na tajiriba na waweze kustaafu baada ya miaka six0 na wakipatikana wanapendelea upande wowote, waachishwe kazi hiyo.

Haki za kimsingi afya ya wananchi, walipendekeza kwamba serikali ihudumie kupitia kwa NHIF na NSSF welfare society. Elimu ya zamani walisema irudishwe, wasichana wapewe haki ya kuridhi. Boda boda wapewe huduma za bima na mafunzo ya uchukuzi na serikali ijenge viwanda vidogo vidogo kama sehemu ya Mumias hapa kuhusu kutengeneza peremende, molasses na fruits ya mayai ili kuajiri vijana na wale vijana ambao serikali haiwezi kuhudumia pia walisema hapa haki za msingi, wapewe pesa kidogo ili kuepuka madawa ya kulevya na njia zingine za usherati. Kisha walisema serikali isimamie bei ya bidhaa muhimu kama vile chumvi, mafuta taa, mbolea na kadhalika. Mengine wataangalia katika hiyo sehemu.

Haki za makundi yanayoweza (inaudible) walipendekeza wakina mama, walemavu na wengine waweze kulindwa na katiba na haki za watoto wasichana hasa. Ardhi; kuna swali muhimu ambalo lilitokezea hapa ambalo nilitaka nitaje kwamba walisema, sole propriety itolewe kwa vyeti vya Title Deeds, ibadilishwe na trusteeship kwa thamiri na waandikishe watu watatu kwenye cheti cha kuruthi shamba ili mama, baba na mtoto wa kwanza waweze kuandikishwa ili kuepuka mambo ya kwenda kwa koti kuweze kumiliki shamba ile. Pia serikali irejeele kufanya ukaguzi wa mashamba upya ili garama za kufanyia survey zimekuwa ngumu zaidi.

Haki ya jamii tofauti tofauti za kitamaduni, nafikiri hayo yatapitiwa lakini walisema katiba ilinde tamaduni za watu kulingana na hali yao na sehemu zao. Mwisho ni sehemu muhimu na ningelisema kwamba walisema katiba isibadilishwe ovyo ovyo na iandikwe kwa lugha zote za makabila ya Kenya ili kufanikisha kuelewa na iweze kugawa kupitia ofisi ya Naibu wa Chief ili wananchi waweze kuisoma na kuielewa, kuanzisha training kuhudumia vyama vya kisiasa na sehemu zingine za katiba ili

wananchi wajue haki zao. Katiba isitumiwe na watu binafsi kuwanyanyasa wengine mbali iwe ni chombo cha utaiifa na watu wachache wasiruhusiwe kumiliki mashamba makubwa makubwa ili hali kungali na squatter nchini. Sehemu kame iweze kuhifadhiwa na katiba itenga hekari fulani za shamba zinazomruhusu mtu kumiliki moja au kampuni au jamii na katiba isiruhusu watu kuzitaja sehemu zao kuwa upande mmoja wa kisiasa ili nchi yote iwe huru watu kudai kura zao. Hayo ndio maoni ya wananchi wa kanda ndogo ya Bukaya. Asanteni

**Com. Raiji:** Commissioners (inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Mwalimu Mkuu kwa hayo yote yako na ya wazee kwani ulisema hii maoni ilikuwa ya wazee. Hao ni wazee wa kike ama wa kiume ndio swali langu la kwanza. Shikilia hayo maswali nitakuuliza maswali kadhaa. Umesema kuwa habari ya wazazi wa kambo iondolewe. (inaudible) hayo nitahitaji unifafanulie kuwa ni vipi kwani baba akiwa na watoto na ameo bibi mwingine, huyo ndio hard work sijui kama hapa kwa Kiluhya kuna mama mwenye watoto huolewa mahali pengine lakini mahali pengine utasikia mama anaweza kuwa na watoto na akaolewa pahali pengine na basi mzazi wa kambo akawa hapo. Sielewi hapa unataka katiba ifanye nini juu ya hili jambo. Umeeleza pia ungetaka kuona mihula miwili tu ya miaka tano. Sikuelewa kama ni kwa Rais peke yake ama ni kwa kila mtu, ama ni kwa madiwana ama kwa wanaBunge. Kwa hivyo pia ningetaka ufafanuzi hapo. Pengine memorandum yako inaeleza viema zaidi.

Umesema pia mama akija na watoto ameolewa nchi nyingine na amekuja na watoto, wapatiwe uraia wa miaka tano wakichunguzwa kama watarudiana. Je, na yule mama ambaye hawachani na bwana yake kwame lakini anataka uraia wa watoto wake wawe pia raia wa Kenya, wazee walisema nini? (inaudible) niliona wazee walikuwa (inaudible). Swali langu la mwisho ni kuhusu vyeti vya kumiliki aridhi. Umesema liandikwe kwa jina la baba na mama na mtoto wa kwanza. Na wale ambao hawapati watoto nafikiri itakuwa na majina yao wawili. Lakini (inaudible) watangoja mpaka wapate mtoto wa kwanza ndio waandikishe mashamba ama, we are looking at the practical history vile tutayafanya hayo mapendekezo kwenye katiba. Pia umesema kuwa watu wasikubalishwe kumiliki ardhi kubwa na wengine huku hawana mashamba. Je, walikuwa wanataka kusema wale wenye watakubaliwa basi kumiliki ardhi wakubalishwe acres ngapi ndio tuweze kufikiria mashamba makubwa zaidi. Hayo ni maswali mengi lakini kwa sababu wewe ni mwalimu, utayakumbuka lakini nitakukumbusha yenye utakuwa umesahau

**Rowland Ombuge:** Natumai kwamba hii karatasi ambayo tumeeleza hii lakini kwanza swali la kwanza lilikuwa kuhusu hali ya mama na baba kambo. Jambo hili wazee na wamama, hatukuwa wazee peke yetu. Waliangalia na wakasema iwapo baba ana wake wawili au pengine mama ameondoka na huyu ameo na wakati tunaanza kuiteka jamii kuanza kubagua kujua hali ya mama kambo na baba kambo, hii ndio inaleta migorogoro hata kwenye taifa, tunaanza kujiona kwa makabila tofauti au uzao wa tumbo fulani fulani. Lakini walifikiria kwamba jamii ichukuliwe kwamba baba na mama. Hata ikiwa mama mmoja alikufa na mwingine akaoleka, yule ni mama na iwe tu ni kwamba watoto wamchukulie yule kama mama yao, vitu vinalete utaiifa pia kuanza kufurugana.

Sehemu ya pili ambayo ulizungumzia, natumai ilikuwa kuhusu hali ya miongo miwili ya miaka minato. Walipendekeza hadi madiwani na hata wakaongeze Mayors wawe na miaka mitano, wajumulishe tu lakini madiwani, Wabunge na Rais, hata WaZiri mkuu iwapo tutaanzisha kifungo hicho, waweze kufunga miaka kumi iwapo watateuliwa tena ili tuweze kuwapa watu wengine nafasi ya kutawala.

Kisha kuna swali kuhusu hali ya mashamba.

**Com. Salome Muigai:** Uraia.

**Rowland Ombuge:** Katika uraia huu ulikuwa ukiuliza kwamba iwapo kuna mama ambaye hajaoleka, sivyo?

**Com. Salome Muigai:** Mama ameoleka, hataki kuachana na bwanake na bwanake ni mgeni ama sio raia wa Kenya na mama anataka watoto wake wawe Wakenya. Nyinyi mlisema nini?

**Rowland Ombuge:** Tulisema hivi katika hii sehemu, watoto wale waandikishwe kwa babu wa Kikenya yaani baba ya mama yule ambaye ni Mkenya lakini watoto wale wawaonyesha kwa ukoo wa Kikenya wa mama kama baba ni wa ugeni na mama anataka wapewe uraia. Wachukuliwe kwamba waandikishwe kwa babu yao ambaye alimzaa mama ili kutambulisha asiria yake hapa Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Hebu mnasema mama hapeani uraia?

**Rowland Ombuge:** Tunachukulia kwamba, walijaribu kuangalia katika sehemu hii na tamaduni za sehemu hii wakisema kwamba, kuna wimbo una sema (Luhya dialect). Mama akioleka kutoka kwao anatoka kutoka katika ile boma na iwapo atarudi, ni babu atawachukua wale watoto akisema watamchinja mbuzi kwa hivyo sasa akiwagawia kitu atawagawia kitu kidogo. Kwa hivyo ndio walisema watoto hao wachukuliwe kwa babu wa Kikenya na baba Mkenya ambaye anawazaa ndio tulisema kwamba achukuliwe kama hawa ni watoto wenye uRais halisi.

Swali lingine lilikuwa kuhusu Trustship na sole Proprietorship. Wamama na wazee waliangalia na wakasema kwamba, huenda mzee afe na isalie mama na mtoto kijana au mama afe na akibakia huyu mmoja na kwa sababu sheria inasema sole proprietor, ndiye mwenye shamba. Lakini wakachukulia wakaona kwamba iwapo baba hajaoa na amenunua shamba, alikuwa akijiandaa kuoia ili anapomuoa mkewe, ichukuliwe hatua kwamba lazima Naibu wa Chief aandikishe watu hawa wameoana na iandikwe kwa land registrar ili mama aingishwe kwenye title deed na iwapo watampata mtoto wa kwanza pia kwa sababu tulisema vyeti vya kuzaliwa vitolewe kupitia ofisi ya Naibu wa Chief. Mtoto huyu aonyeshe kama kiongozi mwenye kumiliki shamba lile ili tusiwe na kung'ang'ania mashamba au watu wa ukoo kuja kung'ang'ania mali na wakati mtu mmoja anapoondoka. Hapo ndio

walikuwa wanazungumzia swali hilo. Sijui kama nimemaliza maswali yote.

**Com Raiji:** Nafikiri saa imekwisha Mwalimu sasa I think you have taken too long

**Rowland Ombuge:** Asante.

**Com Raiji:** We go to the next speaker. Ibrahim Shiundu. Asante sana if you can register (inaudible) Ibrahim Shiundu.

**Ibrahim Shiundu:** Yes.

**Com Raiji:** Mzee karibu. You have five minutes.

**Ibrahim Shiundu:** Hamjambo nyote?

**Audience:** Hatujambo.

**Ibrahim Shiundu:** Bwana Commissioner

.....*End of tape 1 side A*

**Ibrahim Shiundu:** self help group inaitwa Urunga Self Help Group. Memorandum yetu kwa Constitution Review Commission inaguzia mambo manne na mambo yenyewe nitayasoma kwa kimombo. Ya kwanza itashikilia traditional and cultural leadership. Ya pili itakuwa type of governance. Nikienda ya kwanza, I start off by saying we request our honourable government of Kenya to kindly recognize traditional and cultural leadership Constitutionally and prior to coming of the elections.

- This leadership to our constitution and which was wiped by communities concerned which was a clear understanding of the rules governing the area and the relationships for example; elders were for governance, leadership, and district settlement and ensured security for all sectors, men, women and the youth.
- Social and economic welfare of this community, there were Chiefs with power and consority lead under this leader who also acted as a custodian for the community. Like in Western Kenya, we had this kind of traditions and cultural leadership known as ‘Nabongo’ under King Mumia who was famously known or heard of in Kenya and other countries.
- When the colonialists arrived in Kenya, they found Nabongo Mumia ruling this part of this country and Uganda and then entered into a treaty and collaborated and worked together peacefully but could not include his reign or responsibilities into the Constitution thus weakened his power which also happened to our independent Constitution.

- Therefore we request that our current Nabongo is namely Victor Mumia Shitawa to be included in the presently being reviewed Constitution as other countries are having in their Constitution, for example Uganda the Kabaka and then we have first wives, etc. We are sure the traditional and cultural leadership if restored shall not under any circumstance be engaged in politics but might be involved in advisory status within the government and local authorities within the areas where such exists but mostly on matters pertaining to culture, custom and traditions.
- Lastly, when leadership is restored, it shall be used at a large extent to land, domestic and simplistic cases and disputes now congested in our courts. When I go to the second part, the type of government.

**Com. Raiji:** Sorry you need to give us more of recommendations summarized so I will give you a minute to do that because your time is more or less over. On the second point, you can just give me recommendations.

**Ibrahim Shiundu:** A recommendation on the type of government, which we choose, was majimboism and the President to serve 4 years in two terms. The regions to be represented equally and the police force to not to handle people in brutal manner and the landless people to be considered by the government for allocation of land from public lands, from individuals having several huge lands and the state landlessness causes thuggery. That is all I have. Thank you.

**Com Raiji:** There is a clarification

**Speaker:** (inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much for your views. I have one question about the traditional governance. Every place we have gone around Kenya, women have told us that the traditional governance left them out of governance, whether it was village governance, whether it was the Council of Elders or whether it was the traditional Chief, there was no room for governance for women. Now, when you give us this as a recommendation for the Constitution, are you suggesting we create people leaving women out or do you have some interventions that you have gone through that would bring women able leadership?

**Ibrahim Shiundu:** Thank you very much. About women being left out of the governance in our traditional times, we feel during our time, women were treated equally and thus like the inheritance of land we have heard that you were given a portion whereby in that portion of land, it is your children who will inherit. As such, we thought it was a fair deal during those days. Thank you.

**Com. Salome Muigai:** Is that leadership? I am just looking for your thought.

**Ibrahim Shiundu:** When we come to leadership, traditionally in the real sense, it used to be just entirely men alone.



**Com. Salome Muigai:** Do you want us to continue that way?

**Ibrahim Shiundu:** Well, as you see, if there is a new correction we might look at it (inaudible) but what is accepted is men.

**Com Raiji:** Thank you. Can we have Mr Joseph Mukuyu ambaye utafuatwa na Rosemary Obonyo kutoka Maendeleo. Endelea, majina yako kwanza.

**Josephat Wamukoya:** Kwa majina naitwa Josephat Wamukoya Lifutu kutoka Bukaya. Kwanza mimi ni kiwete. Nazungumza kufuatana na vile nilitumwa na viwete wenzangu. Sisi viwete tunasumbuka kwa njia nyingi sana maana ukiwa kiwete, una tumbo na inataka ujaze kitu, utatoa wapi? ukiwa kiwete, una watoto na watasoma namna gani? Ukiwa kiwete wewe unagonjeka, utapelekwa hospitali namna gani? Kwa kila shida inaingilia viwete kwa maana wanapokuwa kwa kila laini hata sura hawana kwa maana yeye ni kiwete.

**Com Raiji:** Sasa unataka tufanye nini?

**Josephat Wamukoya:** Nataka usaidizi. Hata nikiwa na shamba, nitalima namna gani, nione mimi, nina mkono mmoja, nitalima namna gani? Tumbo haikuzeeka

**Com Raiji:** Josephat, vile tunajaribu kufanya ni kusikia maoni yenu vile tunaweze kufanya ili nyinyi msaidike

**Josephat Wamukoya:** Yes. Hiyo ndio imetuma hii venue yenu mtusaidie. Tufanye nini kwa maana ugonjwa uko nyumbani, watoto wako nyumbani, tumbo iko nyumbani, shida iko nyumbani, tufanye namna gani? Mtusaidie.

**Com Raiji:** Okay. Nimesikia hayo, tafadhali jiandikishe. Rosemary A Obonyo.

**Rosemary Obonyo:** Kwa majina naitwa Rosemary A. Obonyo, Maendeleo ya Wanawake Bukaya sub location. Wamama wa maendeleo tulikaa chini tukajadiliana mambo haya. Kwanza tuliongea juu ya Bunge na tukaona kikao cha Bunge kipewe mda kidogo kama miaka nne sio tano. Wamama wapewe six0% ya viti Bungeni. Wamama tena wapewe nadhifa kuu Bungeni na hata serikalini, wasiwachwe tu kufuata waume. Wapewe kulingana na masomo yao. Tena, Wabunge wachaguliwe wale wana masomo ya juu ili wakifika huko wapewe viti kulingana na masomo yao. Kwa mfano, kama ni daktari apewe wizara ya afya, kama ni major apewe wilaya ya ulinzi. Kama amesomea mambo ya ukulima apewe nafasi ya ukulima. Tena tukaonelea Rais akikosa ama akipatikana na kosa lolote apelekwe kotini sio ati yeye ni mkubwa hawezi kupelekwa kotini.

Hapo pia tuliona Mbunge akiwacha chama chake asiingie chama kingine mpaka huo muhula upite. Watu wafanye campaign

bila pesa, wasipatie wananchi pesa, waongee tu zile vitu wataenda kuwafanyia. Viongozi wa vijiji walipwe mishahara wawache kuomba wananchi kitu kidogo. Kwa upande wa masomo, masomo irudishwe kama zamani. Watoto wakisoma mpaka class ya nne, wafanye mtihani wapate cheti, class ya nane wafanye mtihani na wapate cheti. Kidato cha nne wafanye mtihani na wapate cheti. Serikali iangalia skuli za watu binafsi zinaharibu pesa ya wananchi na haisaidii watoto hasa vyo vya watu binafsi. Katiba yetu iangalie sana maana inaharibu pesa ya wananchi na haisaidii.

Harusi ifanywe kanisani na sio kwa ofisi ya DO ili izuie wamama wengi kuwa na vyeti vya harusi kwa mume mmoja. Bibi wengi wafungwe maana inaendesha maovu, hayana maneno ya Mungu. Mila na desturi zote ziachwe kabisa kwa mfano kurithi wanawake mume akifa, wanamletea mwanamume mtoto mdogo na yeye ashazeeka, hii inaharibu maisha ya mtoto. Kutairisha wanawake na vijana kwa kisu iwachwe kabisa. Kurudi kwa matanga mara kwa mara iwachwe na kupeleka watoto vichakani kutairiwa. Hizi zipigwe marufuku na sheria ya tume. Watoto vilema wapewe nafasi katika jamii, wapewe elimu bora na wasibaguliwe. Kutoa mahari isikuweko kabisa maana inafanya waume wanawatesa wanawake ati wamewanunua.

Wanaume wanaopiga wanawake wachukuliwe adhabu kali. Wanaume wanao wanajisi wanawake na watoto wasichana wafinywe. Mwizi akipatikana wazi wazi akatwe mkono mmoja. Kesi ya mashamba irudishwe kwa wazee maana wazee ndio wanajua mpaka ya mashamba. Watoto wote, wasichana na waume wagawanyiwe urithi bila kubagua. Mtu akistaafu, apewe haki yake yote, yaani hata miaka tano bado anangojea hajapata pesa zake. Apewe zote hata akila na kumaliza akufe. Mtu akifa, mkewe aendelee kupata pesa ya pension kwa miaka two1 ili aweze kufundisha watoto ambao amebaki nao. Nikimalizia kama wamama wa South Wanga, tunaomba tume itupatie sehemu yetu ya Bunge kwa hapa ni sehemu kubwa ambayo hatuwezi kupigia Mbunge yule yuko, tunataka Mbunge wetu South Wanga. Mungu awalinde.

**Com Raiji:** Asante mama. Mwingine ni Jackson A Lubare. Jiandikishe huko. Atafuatwa na Martin Oloo. Jackson A Lubare.

**Jackson Lubare:** Wageni wetu ambao wamesimamia tume ya leo, mimi nina mambo sehemu mbili kuhusu kitabu ambacho nimepata hivi, nina maoni ambayo nimetoa lakini kesho nitaleta ripoti kamili kuhusu hii maneno ya kitabu. Jambo la kwanza ni, jina ni Jackson A. Lubare, Box six, Butere. Kuhusu uridhi wa upokeshaji wa uwezo, ni nani anayepasa kuwa na mamlaka ya nchi wakati wa uRais. Nimeonelea ni mkuu wa sheria. La pili, matokeo ya uchaguzi wa Rais itakwazwe vipi? Iwekwe wazi kwa radio, TV na magazeti. Rais aliyekubaliwa aanze kazi yake baada ya uchaguzi mara moja. Rais aliyechaguliwa aapishwe na nani na utaratibu gani ufuatwe? Aapishwe na jaji mkuu na baadaye aletwe katika stadium kuongelesha watu.

Ni katika hatua gani ambayo vifaa vya uwezo vitapokezwa kutoka kwa Rais anayetoka kwa Rais anayeingia? Ni baada ya kuapishwa, Rais anayeondoka akabithi vifaa kwa Rais anayeingia ana kwa ana. Upokezaji wa vifaa vya uwezo uchukue utaratibu gani? Ichukue utaratibu wa kutoka kwa kiongozi hadi mwingine. Je, katiba iweke masharti kwa manufaa ya Rais anayeondoka kuhusu usalama, masilahi, kinga thidi ya mashtaka na mengine? Ndio, lazima apewe usalama, maslahi na kinga

pia. Naingia kwa tume ya katiba ya tahasisi na ofisi. Tunahitaji tume za katiba ya tahasisi na ofisi ikiwa ndio au la. La, katiba ya Kenya ifanywe na mkuu wa sheria. Halafu tuanzishe ofisi ya mkopeshaji mlalamiko, ombudsman ikiwa ndio ofisi hii iwe na uhusiano kali na matawi mengine ya serikali.

Tuunde tume zipi za katiba? Tume ya haki za binadamu lazima iundwe, Tume ya sinsia lazima tuwe nayo, tume ya thidi ya ufisadi lazima tuwe nayo na tume ya ardhi na zingine, tafadhali fafana. Tume ya watoto, ya wananchi, ya wakulima, ya walemavu lazima tuwe nazo. Tume hizo zinaweza kuwa na majukumu gani, inaweza kusaidiwa aje na upande wa Mbunge.

Nikienda upande wa uhusiano wa kimataifa, je utenda kazi wa maswala ya uhusiano wa kimataifa uwe na jukumu la mamlaka ya nchi peke, ikiwa sio ni nani, mwingine anaweza kutekeleza wajibu huo? Iwe ni Bunge. Bunge inaweza kutekeleza jukumu gani ikiwa iko katika utenda kazi wa maswala ya kimataifa? Ni kujali maswala ambayo ni ya anaye husika. Jukumu la Bunge katika kutenda kazi wa maswala ya mitaa itofautishwe vipi ile ya mamlaka ya nchi? Bunge la kazi litilie mkazo kuhusisha wanao husika. Namaliza na je, mafikiano ya mapatano ya kimataifa na maneno yawe ya ardhi na ya moja kwa moja kwa sherehe za nchi ikiwa sio, zinaweza kutengenezwa? Ndio, zitengwe.

Nikienda kwa utawala wa ushirikisha. Je, mashirika yanayokuwa na serikali na makundi mengine yenye utaratibu yana jukumu lolote katika utawala? Ikiwa ndio, jukumu hilo liwe lipi? Ndio afya nchini, mali na elimu. Ni maswala yapi yanayohusu mashirika ya kiraia yanayopasa kushughulikiwa na katiba? Utamaduni na mila. Je, donor ielekezwe uendeshaji wa mashirika ya uraia pamoja na vyombo vya habari? Ndio kwa kuinua uchumu. Je, katiba ithibitishwe jukumu la ushirika wa kiraia ikiwa ndio ni katika umbo fupi kwa ulinzi na kisiasa.

**Com Raiji:** Sema la mwisho, saa inakwisha.

**Jackson ALubare:** La mwisho langu ni maoni kuhusu bendera yetu ya Kenya nataka ibaki hata kama mtu mwingine wa opposition atakuja atumie kwa sababu inatukumbusha sisi wanakenya vile tulipata uhuru. Ya pili, Rais ambaye anataka kuchukua term kuanzia sasa nataka amalize miaka kumi na pesa ambayo itatoka iwe tu muhuri wa Kenya, kichwa cha kiongozi kisiwe katika pesa. La tatu ni, sisi wananchi wa kawaida tuko na shida, mtu akipeleka vitu sokoni hata kama ni mboga ya shilingi hamsini lazima atoe ushuru kwa watu wa county council. Nne ni kuhusu uhuru wa kuabudu. Ni lazima uheshimike na serikali ichunguze. Asante sana, hayo ndio niko nayo mengine nitamaliza kesho.

**Com Raiji:** Okay Jackson, jilandikishe huko. Martin Oloo? Martin Oloo utafuatwa na Rachel Omondi.

**Martin Oloo:** Asante sana Mwenye Kiti. Kwa jina naitwa Martin Oloo ni mkaaji wa Mumias constituency. Kuna mambo machache ambayo ningependa kuguzia, kuna mengine yamesemwa lakini ningependa kuisitiza tu na mniruhusu nitasema kwa lugha ya kimombo. We need a Preamble in our Constitution and basically, it should be able to harmonize the process between

this Constitution review process and the Lancaster House negotiations and recognising the need for a Constitutional review after the various crisis that we have so far gone through. In particular, that Preamble should also address issues of building of the nation, issues of laying foundations of a democratic and open society, issues of improvement of quality of life of all citizens and a release of their potential and also founding the Kenyan nation within an International community of nations so that Preamble should be that clear.

